# RUWAZA ZA KIMOFOLOJIA ZA MAJINA YA MAHALI YA KIHAYA: MTAZAMO WA MOFOLOJIA LEKSIKA

*Adventina Buberwa*

**Ikisiri**

*Makala haya yamechunguza ruwaza za majina ya mahali ya Kihaya[9] kwa kuchanganua vijenzi mbalimbali vinavyojenga majina hayo. Data iliyochunguzwa ni sehemu ya data iliyokusanywa kutoka katika wilaya za Muleba, Missenyi, Bukoba Vijijini na Bukoba Mjini, mkoani Kagera kwa ajili ya tasnifu ya Uzamivu. Uchanganuzi wa data umeongozwa na Nadharia ya Mofolojia Leksika kwa mujibu wa Kiparsky (1982) inayosisitiza kuwa vipashio vinavyounda maneno vimepangwa kidarajia kimsonge ambapo vipashio vidogo huungana ili kuunda vipashio vikubwa. Data za utafiti huu zimewasilishwa kwa kutumia majedwali. Hata hivyo, baadhi ya data zimewasilishwa kwa kutumia michoroti ili kudadavua vyema mpangilio wa vipashio vinavyounda majina husika na kuonesha jinsi vipashio hivyo vilivyopangwa kidarajia kimsonge. Matokeo ya uchanganuzi huo yamedhihirisha kuwa majina ya mahali yaliyochunguzwa yameundwa kwa vijenzi mbalimbali ambavyo vimechanganuliwa kimofolojia. Tofauti na madai ya baadhi ya wanaisimu kuwa majina ya mahali yameundwa na mizizi au mashina tu, makala haya yamethibisha kuwa vipo vipashio maalumu vinavyounda majina ya mahali na vinaweza kuchanganuliwa kimofolojia.*

## 1.0 Utangulizi

Taaluma ya uchanganuzi wa vijenzi vya maneno imewashughulisha wataalamu mbalimbali kwa muda mrefu. Katika miaka ya 1920 hadi 1960 wanamuundo kama vile Ferdinand de Saussure, Edward Sapir, Benjamin Whorf, Leonard Bloomfield walishughulikia sana muundo wa maneno hususan katika kiwango cha mofolojia na walisisitiza kuwa sharti kila kiwango cha lugha kijitegemee. Wataalamu hawa walitambua mofimu kama kipashio kidogo cha kiuchanganuzi kinyume na wanamapokeo waliotazama neno kama kipashio kilicho kidogo zaidi (Nida, 1949). Mofimu moja au zaidi hujenga neno kamili na maneno huunganishwa kwa utumia kanuni za lugha ili kujenga vipashio vikubwa zaidi kama vile maneno ambatani, virai, vishazi na sentensi.

Lugha mbalimbali duniani huwa na vijenzi maalumu vinavyounda maneno. Katika lugha tenganishi (kama Kichina na Kivietinamu) kwa mfano, maneno huundwa kwa neno moja moja bila kuchanganyika na viambishi. Katika lugha ambishi-bainishi kama Kiswahili na Kihaya, maneno huundwa kwa mfuatano bayana wa mofimu. Mofimu hizo huwa na maana na mizizi hudhihirika wazi bila kuchanganyika na viambishi. Mofimu katika lugha ambishi changamani huwa na uamilifu zaidi ya mmoja. Hivyo, mofimu moja kwa mfano, inaweza kuwakilisha

---

[9] Kihaya ni lugha ya Kibantu inayozungumzwa Kaskazini-Mashariki mwa Ziwa Nyanza, Tanzania.

njeo, nafsi, kauli na kadhalika. Aidha, katika lugha kama Kiarabu na Ciruuri, mofimu huchopekwa ndani ya mzizi na huwa vigumu kutenganisha mzizi na viambishi (Mgullu, 1999; Massamba, 2004).

Licha ya lugha za Kibantu kama Kiswahili na Kihaya kutambulika kama lugha ambishi-bainishi, majina ya mahali yamekuwa yakitazamwa kama maneno yaliyoundwa kwa mofimu moja tu na hivyo hakuna utafiti uliochunguza vijenzi vya majina ya mahali hususani majina ya kata, vijiji/mitaa na vitongoji vyake. Ingawa kuna tafiti kadhaa zilizofanywa kuhusu majina ya mahali ya lugha mbalimbali, tafiti nyingi zimefanywa ama kwa kushughulikia asili na maana za majina ya mahali (kwa mfano, Levitt, 1959; Cameron, 1961; Kalkanova, 1999; Kadmon, 2000; Buberwa, 2010 na Elihaki, 2014) au historia ya majina ya mahali (kwa mfano, Dalby, 1984; Diagne, 1984 na Schotsman, 2003). Aidha, baadhi ya watafiti (kama Angus, 2005; Rugemalira, 2005; Rye, 2006; Mphande, 2006; Mojapelo, 2009 na Buberwa, 2011) wamegusia baadhi ya vipengele vya kimofolojia vya majina ya mahali. Hata hivyo, tafiti zilizofanywa kuhusu majina ya mahali kwa mkabala wa kimofolojia si za kina. Inawezekana kuwa labda kutokushughulikiwa kwa suala hili kwa kina kunatokana na madai yaliyowahi kutolewa na baadhi ya wanaisimu kama Agard (1984) na Habwe na Karanja (2007) kuwa nomino mahususi huundwa na mizizi tu, hivyo haziwezi kuchanganuliwa kimofolojia. Kutokana na madai hayo, makala haya yameangazia vijenzi mbalimbali vya majina ya mahali ya Kihaya kwa lengo la kubainisha vijenzi maalumu vya majina ya mahali katika lugha hiyo. Uchanganuzi huo umeongozwa na kiunzi cha Nadharia ya Mofolojia Leksika kwa mujibu wa Kiparsky (1982).

## 2.0 Ufafanuzi kuhusu Nadharia ya Mofolojia Leksika

Mofolojia Leksika ni nadharia zalishi na nyambulishi inayotambua kiwango cha mofolojia kama kiwango mahususi cha lugha. Nadharia hii imejengwa katika misingi ya mkabala unaoitambua mofimu kama kipashio cha msingi cha kiuchanganuzi (Lieber, 1990,1992). Nadharia ya Mofolojia Leksika inaeleza kwamba mofolojia kama sehemu ya lugha imepangwa katika mfuatano wa ngazi kimsonge (Kiparsky, 1982; Katamba, 1993; Macmahon, 2000; Katamba na Stonham, 2006). Hii ina maana kwamba viambishi (mofimu) vinavyopachikwa katika mizizi ili kuunda neno hupangwa kidarajia. Kimsingi, nadharia hii inaonesha uhusiano wa maumbo ya maneno na sheria zinazodhibiti maumbo hayo. Nadharia ya Mofolojia Leksika hutambua viwango viwili vya kanuni ambavyo ni kanuni Leksika ambazo huhusika katika kuunda neno kubalifu kiLeksika na kanuni kirai ambazo hutenda kazi baada ya neno kuundwa.

Nadharia ya Mofolojia Leksika imejengwa katika mihimili mbalimbali kama vile kanuni ya ngazi Leksika, kanuni ya mzunguko kamili, kanuni ya kufuta mabano,

kanuni ya ufinyu wa sifa na kanuni ya kuhifadhi muundo. Kwa kuwa makala haya yanachunguza ruwaza za kimofolojia za majina ya mahali, uchanganuzi wa data umeongozwa na nadharia hii ya Mofolojia Leksika. Msingi wa kuteuliwa kwa nadharia hii ni madai ya mhimili wa kanuni ya ngazi Leksika kwamba maneno huundwa na vipashio mbalimbali na vipashio hivyo vimepangwa katika ngazi kimsonge. Vipashio hivyo huunganishwa hatua kwa hatua na kujenga vipashio vikubwa zaidi. Hivyo basi, nadharia hii ya Mofolojia Leksika imetumika katika kubainisha na kufafanua ruwaza za kimofolojia za majina ya mahali ya Kihaya. Hii imekuwa changamoto kwa baadhi ya wataalamu kama Agard (1984) na Habwe na Karanja (2007) wanaodai kuwa majina ya mahali yameundwa kwa mizizi tu, hivyo hayawezi kuchanganuliwa kimofolojia.

## 3.0 Ngeli za Nomino katika Lugha ya Kihaya

Kwa kuwa lengo la makala haya ni kubainisha vijenzi mbalimbali vinavyounda majina ya mahali ya Kihaya, ni vyema kudokeza kuhusu ngeli za nomino za lugha hiyo. Kuna ngeli za nomino 18 katika lugha ya Kihaya (Byarushengo na wenzie, 1977; Kaji, 2000; Muzale, 2006; Leonard, 2008). Zifuatazo ni ngeli hizo; viambishi-ngeli vyake, mifano kwa kila ngeli na tafsiri ya mifano hiyo:

| KIAMBISHI NGELI | | MIFANO | TAFSIRI |
|---|---|---|---|
| 1 | MU | ***mu-**kazi* | mwanamke/mke |
| 2 | BA | ***ba-**kazi* | wanawake/wake |
| 3 | MU | ***mu-** ti* | mti |
| 4 | MI | ***mi** -ti* | miti |
| 5 | I | ***i-** huli* | yai |
| 6 | MA | ***ma**- huli* | mayai |
| 7 | KI | ***ki-** tebe* | kiti |
| 8 | BI | ***bi** - tebe* | viti |
| 9 | N | *mbwa* | mbwa |
| 10 | N | *mbwa* | mbwa |
| 11 | RU | ***ru-** fu* | kifo/msiba |
| 12 | KA | ***ka-** ti* | kimti |
| 13 | TU | ***tu-** ti* | vimiti/vijiti |
| 14 | BU | ***bu-** so* | uso |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 15 | KU | ***ku-*** *twi* | sikio |
| 16 | HA | *a-* ***ha*** | hapa |
| 17 | KU | ***ku****-li* | kule |
| 18 | MU | *o-****mu****-nda* | ndani |

***Chanzo:*** *Leonard (2008)*

Sehemu hii imeangazia ngeli za nomino katika lugha ya Kihaya. Katika makala haya imebainika kwamba viambishi-ngeli mbalimbali hujitokeza katika majina ya mahali ya Kihaya. Viambishi-ngeli katika majina ya mahali ya Kihaya huchombezwa na nomino za kawaida ambazo kwazo majina ya mahali huundwa (Buberwa, 2011). Maelezo ya kina kuhusu utokeaji wa viambishi-ngeli katika majina ya mahali ya Kihaya yamewekwa katika sehemu ya uchanganuzi wa data katika sehemu zinazofuata. Baada ya kubainisha ngeli za nomino za Kihaya, sehemu inayofuata imeshughulikia uchanganuzi wa vijenzi mbalimbali vinavyounda majina ya mahali ya Kihaya.

## 4.0 Uchanganuzi wa Vijenzi Vinavyounda Majina ya Mahali ya Kihaya

Kwa hakika majina ya mahali ya Kihaya yanaweza kuainishwa katika maumbo ya aina mbili kisintaksia, yaani majina yenye muundo wa neno moja na majina ya mahali yenye muundo wa maneno mawili au zaidi. Hata hivyo, lengo la makala haya ni kushughulikia majina ya mahali yenye muundo wa neno moja pekee. Baada ya kuchunguza data tuliyonayo imebainika kwamba baadhi ya majina ya mahali ya Kihaya yenye muundo wa neno moja hujidhihirisha kama nomino. Aidha, yapo majina kadhaa yanayojibainisha kama vitenzi licha ya kurejelea maeneo mbalimbali. Majina hayo ya mahali yamejengwa kwa vipashio kadha wa kadha ambavyo kwa pamoja vinaungana ili kuunda jina moja la mahali. Sehemu zinazofuata zimeangazia vijenzi mbalimbali vinavyounda majina ya mahali ya Kihaya.

## 4.1 Majina ya Mahali ya Kihaya Yanayojidhihirisha katika Umbo la Nomino

Majina ya mahali ya Kihaya yenye muundo wa nomino yanajidhihirisha katika maumbo ya aina mbili. Maumbo ya aina ya kwanza ni yale yasiyonyambulishwa na maumbo ya aina ya pili ni yale yaliyonyambulishwa. Maumbo ya majina yasiyonyambulishwa huhusisha majina ambayo ni nomino kwa asili yake wakati majina ya mahali yaliyonyambulishwa huhusisha nomino zilizonyambulishwa kutokana na kategoria nyingine za maneno kama vile vitenzi, vivumishi na kadhalika. Majina ya mahali ya Kihaya yanayotokana na nomino kwa asili yake hujibainisha katika maumbo mbalimbali. Maumbo yaliyobainishwa ni pamoja na maumbo yenye kiambishi-ngeli na mzizi [ng+Mz], kiambishi tangulizi, kiambishi

ngeli 1, kiambishi-ngeli 2 na mzizi [kt+ng1+ng2+Mz]. Maumbo haya yameelezwa kwa kina katika sehemu zinazofuata.

### 4.1.1 Muundo wa Kiambishi-ngeli na Mzizi [ng + Mz]

Majina ya mahali ya Kihaya katika kategoria hii yameundwa na kiambishi-ngeli na mzizi kama mifano katika Jedwali 1 linavyoonesha:

**Jedwali 1: Mifano ya Majina ya Mahali yenye Muundo wa [ng +Mz]**


| Na. | Majina | Vijenzi vyake | Tafsiri ya Kiswahili |
|---|---|---|---|
| 1. | *Kigemu* | Ki-gemu<br>ng7 -Mz | Mgomba mkubwa |
| 2. | *Kagemu* | Ka - gemu<br>ng12 - Mz | Mgomba mzuri |
| 3. | *Buyango* | Bu – yango<br>ng14 - Mz | Mahali wanapoishi watu wa ukoo wa Bayango |
| 4. | *Nyanga* | N- yanga<br>ng9/10 - Mz | Kaburi |
| | *Mishenye* | Mi – shenye<br>ng4- Mz | Mchanga (wingi) |

**Chanzo**: Uwandani

Mifano katika Jedwali 1 inaonesha kuwa majina ya mahali ya Kihaya yenye muundo wa kiambishi-ngeli na mzizi yameundwa na viambishi-ngeli tofauti tofauti. Viambishi hivyo ni **ki-** (ngeli ya 7) kama inavyoonekana katika mfano wa (1), **ka-** (ngeli ya 12) katika mfano wa (2) na **bu-** (ngeli ya 14) katika mfano wa (3). Viambishi-ngeli vingine ni **n-** (ngeli ya 10) katika mfano wa (4) na **mi-** (ngeli ya 4) kama inavyojitokeza katika mfano wa (5). Kama safu ya tafsiri inavyoonesha katika Jedwali 1, kiambishi-ngeli **ki-** kinadokeza ukubwa, kiambishi **ka-** kinadokeza uzuri, kiambishi **mi-** kinadokeza wingi. Kiambishi **bu-** katika mfano wa (3) kinadokeza dhana ya umahala wakati kiambishi **n-** kimejitokeza katika nomino zisizokuwa na maumbo dhahiri ya umoja na wingi. Kwa mujibu wa taarifa zilizokusanywa uwandani, majina hayo yalitokana na vitu vyenye sifa ya ama udogo, uzuri, ukubwa au wingi wa vitu ambavyo vilikuwapo katika eneo linalohusika.

Kwa ujumla, majina ya mahali ya Kihaya yenye muundo wa kiambishi-ngeli na mzizi yamedhihirisha wazi kuwepo kwa vipashio mbalimbali vinavyoungana ili kuunda neno linalohusika. Hivyo, uchanganuzi wa vipashio vinavyounda majina ya mahali unaongozwa na kanuni ya ngazi Leksika kwa lengo la kubainisha vijenzi mbalimbali vya majina ya mahali ya Kihaya. Kwa hiyo, vipashio vinavyounda majina ya mahali yenye muundo wa kiambishi-ngeli na mzizi vimepangwa kimsonge kama Kielelezo kifuatacho kinavyoonesha:

**Kielelezo 1: Uundaji wa Majina ya Mahali ya Kihaya Kimsonge**




Kama Kielelezo 1 kinavyoonesha majina ya mahali ya Kihaya yenye muundo wa kiambishi-ngeli na mzizi yameundwa na vipashio vilivyopangwa kimsonge kama Nadharia ya Mofolojia Leksika inavyoeleza.

### 4.1.2 Muundo wa Kiambishi tangulizi, Kiambishi ngeli 1, Kiambishi ngeli 2 na Mzizi [kt+ng1+ng2+Mz]

Baadhi ya majina ya mahali ya Kihaya yenye muundo wa neno moja yameundwa na kiambishi tangulizi, kiambishi-ngeli cha kwanza, kiambishi-ngeli cha pili na mzizi. Mifano ifuatayo inawakilisha majina yote yaliyokusanywa yenye muundo huu:

**Jedwali 2: Mifano ya Majina ya Mahali yenye Muundo wa kt+ng1+ng2+Mz**

| Na. | Jina la Mahali | Vijenzi vyake | Tafsiri ya Kiswahili |
|---|---|---|---|
| 1. | *Omurubaale* | o-mu-ru-baale<br>kt-ng18-ng11-Mz | Ndani ya mawe madogo madogo |
| 2. | *Omubilamura* | o-mu-bi-lamura<br>kt-ng18-ng8-Mz | Ndani ya mimea ambayo hutumika kama mipaka |
| 3. | *Omukashenye* | o-mu-ka-shenye<br>kt-ng18-ng12-Mz | Ndani ya mchanga mzuri |
| 4. | *Ahamushenyi* | a-ha-mu-shenye<br>kt-ng16-ng3-Mz | Kwenye mchanga |
| 5. | *Ahakibati* | a-ha-ki-baati<br>kt-ng16-ng7-Mz | Kwenye bati kubwa (jengo la mabati walilojengewa wakimbizi wakati wa vita vya Tanzania na Uganda |

**Chanzo**: Uwandani

Kama mifano inavyoonekana katika Jedwali 2 majina ya mahali katika kategoria hii yameundwa na viambishi tangulizi **a-** na **o-**. Kama zilivyo lugha nyingi za Kibantu, Kihaya pia kina viambishi tangulizi. Katika lugha ya Kihaya kuna viambishi tangulizi vya aina tatu ambavyo ni **a-**, **e-** na **o-**. Hata hivyo, viambishi

tangulizi vinavyojitokeza katika majina ya mahali ya Kihaya ni **a-** na **o-** tu. Kiambishi tangulizi **a-** huambatana na kiambishi-ngeli cha mahali **ha-** wakati kiambishi tangulizi **o-** kinaambatana na kiambishi-ngeli cha mahali **mu-**. Mazingira haya yanaweza kufafanuliwa kwa kutumia kanuni zifuatazo:

**[a-] ⟶ ----------------ha-**
**[o-] ⟶ ---------------mu-**

Kanuni hizi zisomeke kuwa kiambishi tangulizi **a-** hujitokeza katika mazingira ya kufuatiwa na kiambishi-ngeli cha mahali **ha-** wakati kiambishi tangulizi **o-** hutokea katika mazingira ya kufuatiwa na kiambishi-ngeli cha mahali **mu-**. Hii ina maana kwamba kutokea kwa viambishi tangulizi katika majina ya mahali ya Kihaya hutegemea kutokea kwa viambishi-ngeli vya mahali. Ni wazi kuwa katika majina ya mahali ya Kihaya yaliyokusanywa hakuna jina lenye kiambishi tangulizi pekee bila kiambishi-ngeli cha mahali wala kiambishi-ngeli cha mahali pekee bila kiambishi tangulizi. Kwa hiyo basi, vipashio hivi hutegemeana na kukamilishana katika kutimiza lengo la kuunda majina ya mahali ya Kihaya.

Zaidi ya hayo data katika Jedwali la (2) inaonesha kuwa majina ya mahali ya Kihaya katika kategoria hii yameundwa na viambishi-ngeli viwili tofauti. Katika mfano wa (1) kuna ngeli ya 18 na ngeli ya 11 na katika mfano wa (2) kuna ngeli ya 18 na ngeli ya 8. Pia, katika mfano wa (3) kuna ngeli ya 18 na ngeli ya 12. Mfano wa (4) kuna ngeli ya 16 na ngeli ya 3 na katika mfano wa (5) kuna ngeli ya 16 na ngeli ya 7. Utokeaji wa viambishi-ngeli viwili katika jina moja umeonekana katika majina ya mahali yenye viambishi tangulizi tu. Kwa msingi huo, upo uhusiano kati ya viambishi tangulizi na mazingira ya kutokea kwa viambishi-ngeli viwili. Uhusiano huu unaweza kufafanuliwa katika kanuni ifuatayo:

**[ng1 + ng2] ⟶ [a-/o-]-------------------**

Kanuni hii isomeke kuwa viambishi-ngeli viwili hutokea katika jina moja la mahali katika mazingira ya kutanguliwa na kiambishi tangulizi **a**- au **o-**.

Kama mifano iliyowasilishwa inavyoonesha, ni dhahiri kuwa majina ya mahali katika kategoria hii yameundwa na vipashio vidogo vidogo ambavyo kwa pamoja vimeunda jina linalohusika. Vipashio hivyo ni viambishi tangulizi, viambishi-ngeli na mzizi. Kwa hakika Nadharia ya Mofolojia Leksika inadhihirisha ubora wake hususani kuhusu uundaji wa leksimu ambao huzingatia vipashio vidogo kuungana na kuunda vipashio vikubwa.

## 4.2 Majina ya Mahali Nyambulishi

Baadhi ya majina ya mahali ya Kihaya yaliyokusanywa yametokana na vitenzi. Tofauti na majina mengine yaliyoshughulikiwa awali, majina ya mahali katika kategoria hii yameundwa kutokana na unyambulishaji wa vitenzi. Majina ya mahali yanayotokana na vitenzi yanajidhihirisha katika miundo mitatu tofauti ambayo ni muundo wa kiambishi-ngeli, mzizi na kiambishi nominishi [ng +Mz+K/no], muundo wa kiambishi-ngeli, mzizi, kiambishi cha utendea na kiambishi nominishi [ng+Mz+tda+K/no] na muundo wa kiambishi tangulizi, kiambishi-ngeli1, kiambishi-ngeli 2, mzizi, kiambishi cha utendea na kiambishi nominishi [kt+ng1+ng2+Mz+tn+tda+K/no]. Miundo hii inafafanuliwa katika sehemu zinazofuata.

### 4.2.1 Muundo wa Kiambishi-ngeli, Mzizi na Kiambishi Nominishi [ng+Mz+K/no]

Katika data tuliyonayo imebainika kwamba baadhi ya majina ya mahali yanayotokana na mashina au mizizi ya vitenzi hujidhihirisha katika muundo wa kiambishi-ngeli, mzizi na kiambishi nominishi kama mifano katika Jedwali 3 inavyoonesha:

**Jedwali 3: Mifano ya Majina ya Mahali yenye Muundo wa [ng+Mz+K/no]**


| Na. | Majina ya mnyambuo | Vijenzi vyake | Tafsiri ya Kiswahili | Shina la kitenzi |
|---|---|---|---|---|
| 1. | *Irango* | i-rang-o<br>ng5-Mz-K/no | tangazo | -*ranga*-tangaza |
| 2. | *Butembo* | bu-temb-o<br>ng14-Mz-K/no | mahali pa kupanda | -*temba*-panda |
| 3. | *Muteebi* | mu-teeb-i<br>ng1-Mz-K/no | anayetega mitego | -*teeba*-tega |
| 4. | *Kitambo* | ki-tamb-o<br>ng7-Mz-K/no | kafara | -*tamba*-tambika |

**Chanzo**: Uwandani

Katika kategoria hii ya majina ya mahali kama yanavyoonekana katika Jedwali 3 majina yameundwa kutokana na unyambulishaji wa vitenzi ambapo viambishi-ngeli na viambishi nominishi vimeshirikiana ili kuunda majina yanayohusika. Viambishi nominishi vinavyojenga majina hayo ni kiambishi nominishi **-i** na kiambishi nominishi **–o** ambavyo vimepachikwa baada ya mzizi wakati viambishi-ngeli vimepachikwa kabla ya mzizi. Kwa mujibu wa Nadharia ya Mofolojia Leksika viambishi hivi vinawekwa katika kundi la viambishi vyenye athari, yaani viambishi ambavyo husababisha badiliko la kiumbo hivyo kusababisha badiliko la kidhana. Aidha, majina ya mahali katika kategoria hii yameundwa na vipashio vidogo vidogo ambavyo kwa pamoja vimeunda majina ya mahali kupitia katika

mchakato wa unyambulishaji unaozingatia kanuni dhahiri ambao hutokea katika ngazi Leksika ya pili. Vipashio vinavyounda majina yenye muundo wa kiambishi-ngeli, mzizi na kiambishi nominishi vimepangwa katika ngazi Leksika na kudhihirisha muundo ufuatao:

**Kielelezo 2:** ***Mpangilio wa vipashio kimsonge katika muundo wa [ng+Mz+K/no]***




Kielelezo hiki kinafasiliwa kuwa majina ya mahali katika kategoria hii yametokana na mashina ya vitenzi. Hivyo basi, shina la kitenzi huundwa kwanza na kisha kupitishwa katika ngazi ya pili ambapo viambishi awali na viambishi nominishi hupachikwa katika shina husika. Upachikaji wa viambishi hivyo hutokana na mchakato wa unyambulishaji dhahiri ambao kwa mujibu wa Nadharia ya Mofolojia Leksika hufanyika katika ngazi ya pili. Kwa hivyo, viambishi-ngeli na viambishi nominishi hushirikiana katika kuunda majina ya mahali yanayotokana na unominishaji. Kama Kielelezo 2 kinavyoonesha vipashio vinavyojenga maumbo mbalimbali ya majina ya mahali vimepangwa kimsonge hatua kwa hatua ili kukamilisha azma ya kuunda jina kubalifu.

### 4.2.2 Muundo wa Kiambishi-ngeli, Mzizi, Kiambishi cha Kutendea na Kiambishi Nominishi [ng + Mz+ tda+ K/no]

Baada ya kuchunguza data tuliyonayo imedhihirika kwamba baadhi ya majina ya mahali ya Kihaya yana muundo wa kiambishi-ngeli, mzizi, kiambishi cha kutendea na kiambishi nominishi kama mifano katika Jedwali (4) inavyoonesha:

**Jedwali 4: Mifano ya Majina ya Mahali yenye Muundo wa [ng + Mz+ tda+ K/no**


| Na. | Majina ya mnyambo | Vijenzi vyake | Tafsiri ya Kiswahili | Shina la kitenzi |
|---|---|---|---|---|
| 1. | *Kagabiro* | ka-gab-ir-o ng12-Mz-tda-K/no | mahali pa kugawia/kutoa sadaka kwa miungu | gaba-gawa |
| 2. | *Katerero* | ka-teer-er-o ng12-Mz-tda-o | mahali pa kupigia | teera-piga |
| 3. | *Kasherero* | ka-sher-er-o ng12-Mz-tda-K/no | mahali pa kutabiria nuksi | shera-tabiri nuksi |
| 4. | *Bushohorero* | bu-shohol-er-o ng14-Mz-tda-K/no | mahali pa kutokea | shohola-toka/ tokeza |

**Chanzo:** Uwandani

Kutokana na mifano hii wakilishi, majina ya mahali katika kategoria hii yameundwa na viambishi-ngeli mbalimbali kama vile **ka-** na **bu-**. Aidha, viambishi vya utendea **-er-** na **-ir-** vimejitokeza kabla ya kiambishi nominishi **-o**. Kama ilivyoelezwa awali majina haya ya mahali yanatokana na mashina ya vitenzi (tazama safu ya shina la kitenzi katika Jedwali 4). Majina ya mahali yaliyoundwa katika sehemu hii yanadokeza dhana ya matumizi ya eneo husika linalorejelewa. Hoja hii inathibitishwa na maelezo yaliyotolewa katika safu ya tafsiri ya Kiswahili katika Jedwali la 4.

Kama yalivyo majina ya mahali yaliyoshughulikiwa awali, majina haya ya mahali yameundwa na vipashio vilivyopangwa kimsonge kupitia katika ngazi Leksika kama Kielelezo kifuatacho kinavyoonesha:

**Kielelezo 3:** ***Mpangilio wa vipashio kimsonge katika muundo wa [ng+Mz+tda+K/no]***



Kielelezo hiki kinafasiliwa kuwa majina ya mahali katika kategoria hii yametokana na mashina ya vitenzi. Hivyo basi, shina la kitenzi huundwa kwanza na kisha kupitia katika mchakato wa unyambulishaji tendea katika ngazi ya kwanza kabla ya kupitishwa katika ngazi ya pili ambapo viambishi awali na viambishi nominishi hungoekwa katika mzizi husika. Ungoekaji wa viambishi hivyo hutokana na mchakato wa unyambulishaji dhahiri ambao kwa mujibu wa Nadharia ya Mofolojia Leksika hufanyika katika ngazi ya pili (Kiparsky, 1982). Kwa hakika uundaji wa majina ya mahali huzingatia upangaji wa vipashio kimsonge kupitia katika ngazi Leksika zinazohusika.

### 4.2.3 Muundo wa Kiambishi tangulizi, Viambishi-ngeli Viwili, Mzizi, Kiambishi cha Kutendana, Kiambishi cha Kutendea na Kiambishi Nominishi [kt+ng1+ng2+Mz+tdn+tda+K/no]

Majina ya mahali katika kategoria hii yameundwa na vipashio mbalimbali ambavyo kwa pamoja vinaunda jina moja la mahali. Tofauti na majina ya mahali yanayotokana na vitenzi yaliyoshughulikiwa katika sehemu zilizotangulia, majina ya mahali katika kategoria hii yamedhihirisha ruwaza changamani zaidi kwani jina moja lina vipashio kati ya saba (7) hadi tisa (9) kama mifano katika Jedwali (46) inavyoonesha.

**Jedwali 5: Mifano ya Majina ya Mahali yenye Muundo wa [kt+ng1+ng2+Mz+tdn+tda+K/no]**


| Na. | Majina ya mnyambuo | Vijenzi vyake | Tafsiri ya Kiswahili | Shina la kitenzi |
|---|---|---|---|---|
| 1. | *Omwishuuraniro* | o-mu-i-shuur-an-ir-o Kt-K/ng18-ng5-Mz-tdn-tda-K/no | mahali pa kusalimiana | *shuura*-salimia |
| 2. | *Omwiteeraniro* | o-mu-i-teer-an-ir-o kt-ng18-ng5-tdn-tda-K/no | mahali pa kukutania | *teerana*-kutana |
| 3. | *Omwitemanganiro* | o-mu-i-tem-ang-an-ir-o kt-ng18-ng5-Mz-tdn1-tdn2-tda-K/no | mahali pa kukatana | *tema*-kata |
| 4. | *Omwimiriranganiro* | o-mu-i-mir-ir-ang-an-ir-o kt-ng18-ng5-Mz-tda1-tdn1-tdn2-tda2-K/no | mahali pa kumezeana | *mira*-meza |

**Chanzo**: Uwandani

Majina ya mahali katika mifano (1) na (2) yanadhihirisha maumbo yanayofanana kwani ni vipashio saba tu vinavyounda majina hayo ambavyo ni kiambishi

tangulizi, viambishi-ngeli viwili, mzizi, kiambishi cha utendana, kiambishi cha utendea na kiambishi nominishi. Majina haya kama yalivyo majina ya mahali katika sehemu iliyotangulia yanatokana na mashina ya vitenzi. Mchakato wa uundaji wa majina haya hautofautiani sana na ule uliojadiliwa katika sehemu ya (3.1.2.2) ya makala haya. Shina la kitenzi huundwa kwanza kisha kupitishwa katika mchakato wa unyambulishaji ghairi ambao hutokea katika ngazi ya kwanza. Katika ngazi hiyo unyambulishaji tendana na unyambulishaji tendea hufanyika. Viambishi tangulizi, ngeli na viambishi nominishi hupachikwa katika shina la kitenzi katika ngazi ya pili ambayo huhusika na unyambulishaji dhahiri. Vipashio vinavyounda majina ya mahali katika mifano (1) na (2) vimepangwa kimsonge kama Kielelezo 4 kifuatacho kinavyoonesha:

**Kielelezo 4: Mpangilio wa Vipashio Vinavyounda Majina ya Mahali katika Mifano (1) na (2).**




Tukiacha mpangilio wa vipashio vya majina ya mahali katika mifano (1) na (2), mifano (1) - (4) inadhihirisha kuwa unyambulishaji uliofanyika umesababisha baadhi ya sauti kuathirika. Katika mifano ya majina hayo kama ilivyowasilishwa

katika safu ya majina ya mnyambuliko irabu [u] haidhihiriki wazi kutokana na mchakato wa kifonolojia unaojulikana kama uyeyushaji. Uyeyushaji ni mchakato wa kifonolojia ambao huhusika na ubadilishaji wa irabu [u] kuwa kiyeyusho pale inapotokea katika mazingira ya kukabiliana na irabu isiyofanana nayo (Massamba, 2004). Kutokana na mchakato huo tunapata majina kama Om**w**iteeraniro badala ya Om**u**iteeraniro. Kwa mujibu wa Nadharia ya Mofolojia Leksika, mabadiliko haya yanatazamwa kama uhusiano uliopo baina ya mofolojia na fonolojia katika mchakato wa unyambulishaji. Inaelezwa kuwa wakati wa unyambulishaji huwa kuna sauti zinaathirika hivyo kusababisha badiliko la kiumbo katika maneno yanayonyambulishwa (Kiparsky, 1982; Katamba, 1993). Ni dhahiri kuwa Nadharia ya Mofolojia Leksika inatenda kazi hata katika mfumo wa uundaji wa majina ya mahali ya Kihaya.

Ruwaza nyingine zinazojitokeza katika data yetu iliyowasilishwa katika Jedwali (5) ni kutokea kwa viambishi viwili tofauti vinavyodokeza dhana ya kutendana. Viambishi hivyo ni **-ang-** na **-an-** ambavyo vimejitokeza katika mifano (3) na (4). Viambishi hivi vinaambatana kabla ya kiambishi cha utendea kutokea ambapo kiambishi **-ang-** hutangulia na kiambishi **-an-** kufuata. Jambo la kushangaza ni kwamba kiambishi **-an-** hujitokeza peke yake katika baadhi ya vitenzi kama katika mifano (1) na (2). Hata hivyo, hakuna mazingira ambamo kiambishi **-ang-** kinajitokeza peke yake bila kiambishi **-an-**. Utokeaji wa viambishi hivyo katika vitenzi ni wa kiuteuzi kwani baadhi ya mashina machache ya vitenzi huteua kiambishi **-an-** pekee kudokeza dhana ya kutendana. Vitenzi hivyo vikiteua kiambishi **-ang-** maana inayokusudiwa hupotea. Kiambishi **-an-** ni zalishi pale kinapotokea pamoja na kiambishi **-ang-** kwa pamoja katika shina moja la kitenzi. Kwa upande wa kiambishi **-ang-** hakiwezi kutokea peke yake bila kiambishi **-an-**.

Kwa upande mwingine, viambishi vya utendea vimejitokeza mara mbili katika jina moja kama inavyoonekana katika mfano wa (4) katika Jedwali (5). Kiambishi **-ir-** kinachotokea kabla ya kiambishi cha kutendana kinadokeza dhana ya kumtendea jambo mtu au kitu fulani wakati kiambishi **ir-** kinachotokea baada ya kiambishi cha kutendana kinadokeza dhana ya umahali, yaani mahali tukio au jambo lilipofanyika. Japokuwa viambishi hivyo vinadhihirisha umbo la aina moja, uamilifu wa maumbo hayo ni tofauti.

Uchanganuzi uliofanywa kuhusu majina ya mahali ya Kihaya yenye muundo wa nomino umeonesha kuwa majina ya mahali ni leksimu zilizoundwa na vipashio mbalimbali vilivyopangwa kimsonge. Maumbo mengine ni sahili lakini baadhi yamesukwa kwa namna ambayo ni vigumu kuyabaini bila kuhusisha taarifa za wazawa. Ni wazi kuwa kuyatazama majina ya mahali hususani ya Kibantu kama mofimu huru zisizoweza kuchanganuliwa zaidi kimofolojia ni kuficha hazina ya maarifa kuntu yahusuyo isimu ya majina ya mahali ya jamii inayohusika.

Baada ya kuchunguza majina ya mahali ya Kihaya yanayojidhihirisha kama nomino, katika sehemu inayofuata tumeangazia vipashio vinavyounda majina ya mahali yenye muundo wa vitenzi.

### 4.3 Majina ya Mahali yenye Muundo wa Vitenzi

Baada ya kuchunguza data tuliyonayo imebainika kuwa baadhi ya majina ya mahali ya Kihaya kama yalivyo majina ya mahali ya Kiswahili, yana muundo wa vitenzi. Majina haya yamedhihirisha ruwaza mbalimbali za vitenzi licha ya kurejelea mahali fulani. Ruwaza hizo ni kama vile viambishi nafsi, mzizi wa kitenzi, viambishi vya ukanushi, viambishi nyambulishi vya kutendana, kutendwa na kadhalika. Majina ya mahali ya kategoria hii yamegawanywa katika makundi matano (5) kulingana na idadi ya vipashio vinavyounda majina hayo. Makundi hayo yamejadiliwa katika sehemu zinazofuata.

#### 4.3.1 Muundo wa Kiambishi cha Upatanisho wa Kisarufi, Mzizi na Irabu Ishilizi [uk+Mz+I]

Ujenzi wa majina ya mahali ya Kihaya ya kundi hili umezingatia viambishi nafsi na mizizi ya vitenzi. Mifano ifuatayo inawakilisha majina ya mahali yenye muundo huu:


**Jedwali 6: Mifano ya majina ya mahali yenye Muundo wa [uk+Mz+I]**

| Na. | Majina ya mahali | Vijenzi vyake | Tafsiri ya Kiswahili |
|---|---|---|---|
| 1. | *Muleeba* | mu-leeb-a<br>uk-Mz-I | mnaangalia |
| 2. | *Bugasha* | bu-gash-a<br>uk-Mz-I | wa (dogo) nafaa |
| 3. | *Bushagara* | bu-shagar-a<br>uk-Mz-I | wa (dogo) nasindikiza |
| 4. | *Mugaba* | mu-gab-a<br>uk-Mz-I | mnagawa |

**Chanzo**: Uwandani

Mifano katika Jedwali (6) ni vitenzi ambavyo kwa hakika siyo rahisi kugundua kama ni majina endapo taarifa za wazungumzaji wa lugha hazitazingatiwa. Kwa mujibu wa nadharia ya Mofolojia Leksika, vipashio vinavyounda maneno vimepangwa kidarajia kimsonge, kipashio kimoja na kingine huungana ili kuunda kipashio kikubwa zaidi. Majina ya mahali ya kundi hili pia yamedhihirika kuundwa kimsonge kama kielelezo kifuatacho kinavyoonesha:

**Kielelezo 5: Uundaji wa Majina ya Mahali yenye Muundo wa uk +Mz+I] Kimsonge**




Kielelezo hiki kinaonesha kuwa licha ya majina ya kundi hili kuwa vitenzi, muundo wake umezingatia upangaji wa vipashio kimsonge kwa kufuata ngazi Leksika maalumu. Hivyo basi, vipashio vidogo ambavyo ni mzizi **–gash-** na irabu ishilizi **-a** vimeungana kuunda shina la kitenzi ‘**gasha**’ na kiambishi nafsi **bu-** kimeungana na shina la kitenzi ‘**gasha**’ kuunda kitenzi *bugasha* ambacho kinatumika kama jina la mahali.

### 4.3.2 Muundo wa Kiambishi cha Upatanisho wa Kisarufi, Kiambishi Kanushi, Mzizi na Irabu Ishilizi [uk+K/kn+Mz+I]

Majina ya mahali katika kategoria hii yanajidhihirisha katika muundo wa vitenzi vyenye viambishi vya upatanisho wa kisarufi, kiambishi kanushi, mzizi na irabu ishilizi kama mifano katika Jedwali lifuatalo inavyoonesha:


**Jedwali 7: Mifano ya Majina ya Mahali yenye Muundo wa [uk+K/kn+Mz+I]**

| Na. | Majina ya Mahali | Vijenzi vyake | Tafsiri ya Kiswahili |
|---|---|---|---|
| 1. | *Mutashweeka* | mu-ta-shweek-a<br>uk-K/kn-Mz-I | msifunike |
| 2. | *Butagarama* | bu-ta-garam-a<br>uk-K/kn-Mz-I | wasiolala chali |
| 3. | *Butanywa* | bu-ta-nyw-a<br>uk-K/kn-Mz-I | wasiokunywa |

**Chanzo:** Uwandani

Katika mifano hii inaonekana kwamba majina ya mahali ya kategoria hii yanajibainisha katika muundo wa vitenzi. Kama mifano inavyoonekana katika Jedwali hapo juu, majina ya mahali ya kategoria hii yanalenga kudokeza sifa au tabia za watu waliokuwa wakiishi au wanaoishi katika maeneo yanayohusika. Aidha, majina ya mahali ya kategoria hii yanadhihirisha kuundwa kwa vipashio vidogo vidogo ambavyo kwa pamoja vinaunda kipashio kikubwa zaidi kama Nadharia ya Mofolojia Leksika inavyofafanua. Vipashio vinavyounda majina hayo vimepangwa kidarajia kimsonge kama inavyoonekana katika Kielelezo kifuatacho:

**Kielelezo 6: Mpangilio wa Vipashio Kimsonge katika Majina ya Mahali yenye muundo wa [uk+K/kn+Mz+I]**




Kielelezo hiki kinafafanua kuwa vipashio vidogo kama vile kiambishi cha upatanisho wa kisarufi **bu-** na kiambishi cha ukanushi **–ta-** vimeshirikiana na mzizi wa kitenzi **–nywa-** na irabu ishilizi **–a** kuunda kitenzi ambacho kimetumika kama nomino ya mahali. Uundaji wa majina ya mahali unaojielekeza katika muundo wa

vitenzi unaibua hoja kuwa uteuzi wa majina ya mahali hauzingatii kategoria maalumu za maneno. Mchakato huo unaongozwa na masuala ya kimuktadha na hivyo majina ya mahali hayaundwi kinasibu kama kategoria nyingine za maneno.

### 4.3.3 Muundo wa Kiambishi cha Upatanisho wa Kisarufi, Mzizi, Irabu ishilizi, Kiambishi elezi cha namna [uk+Mz+I+Ke/nm]

Majina ya mahali yenye muundo huu pia ni moja ya kategoria iliyopatikana katika majina ya mahali yaliyokusanywa katika maeneo yaliyoteuliwa. Mifano katika Jedwali lifuatalo inawakilisha majina ya mahali yenye muundo wa kiambishi cha upatanisho wa kisarufi, mzizi, irabu ishilizi na kiambishi elezi cha namna:


**Jedwali 8: Mifano ya Majina ya Mahali yenye Muundo wa [uk+Mz+I+Ke/nm]**

| Na. | Majina ya Mahali | Vijenzi vyake | Tafsiri ya Kiswahili |
|---|---|---|---|
| 1. | *Butuurage* | bu-tuur-a-ge<br>uk-Mz-I-Ke/nm | wanapoishi vizuri |
| 2. | *Mugirage* | mu-gir-a-ge<br>uk-Mz-I-Ke/nm | mnafanya vizuri |
| 3. | *Baijage* | ba-ij-a-ge<br>uk-Mz-I-Ke/nm | wamekuja vizuri |

**Chanzo:** Uwandani

Mifano ya kategoria hii inaonesha kuwa vitenzi husika vimeteuliwa kwa sababu vinadokeza namna watu wa eneo husika wanavyofanya mambo au wanavyoishi. Dhana hii inadokezwa na kiambishi elezi cha namna **-ge** ambacho kimengoekwa baada ya irabu ishilizi. Uundaji wa majina haya pia umeongozwa na mhimili wa nadharia ya Mofolojia Leksika unaozingatia kuwa leksimu huundwa na vipashio vidogo vidogo ambavyo vimepangwa katika ngazi Leksika kimsonge. Kielelezo kifuatacho kinawakilisha mpangilio wa vipashio kimsonge katika majina ya mahali yenye muundo wa [uk+Mz+I+Ke/nm]:

**Kielelezo 7: Mpangilio wa Vipashio Kimsonge katika Majina ya Mahali yenye Muundo wa [uk+Mz+I+Ke/nm]**




Kielelezo hiki kinadhihirisha kuwa majina ya mahali ya kategoria hii yameundwa na vipashio vilivyopangwa kimsonge ambapo vipashio vidogo vimeungana na kuunda kipashio kikubwa zaidi. Hivyo basi, ni wazi kuwa majina ya mahali hayaundwi na maumbo yasiyoweza kuchanganuliwa kimofolojia kama baadhi ya wanamofolojia wanavyodhani.

### 4.3.4 Muundo wa Kiambishi cha Upatanisho wa Kisarufi, Kiambishi kanushi, Mzizi, Kiambishi cha Kutendana na Irabu Ishilizi [uk+K/kn+Mz+dtn+I]

Pamoja na ruwaza mbalimbali za majina ya mahali ambazo zimejadiliwa awali, imebainika kuwa jina moja la mahali kati ya majina yenye muundo wa kitenzi limeonekana kuwa na muundo wa tofauti na ruwaza zilizotangulia. Jina hilo la mahali lina muundo wa kiambishi cha upatanisho wa kisarufi, kiambishi kanushi, kiambishi cha kutendana na irabu ishirizi. Chunguza jina lifuatalo:

Bu-ta-ganj-an-a wasiopendana
uk-K/kn-Mz-tdn-I

Licha ya kuwa na muundo wa jinsi hii, muundo huu si zalifu kwani kati ya majina ya mahali yenye muundo wa kitenzi yaliyokusanywa katika wilaya zote nne jina moja tu ndilo lililodhihirisha muundo huo.

### 4.3.5 Muundo wa Kiambishi cha upatanisho wa kisarufi, Kiambishi kanushi, Mzizi, Kiambishi cha utendwa na Irabu Ishilizi [ng+K/kn+tdw+I]

Katika utafiti huu imebainika kuwa kuna majina ya mahali yenye muundo wa kiambishi cha upatanisho wa kisarufi, kiambishi kanushi, mzizi, kiambishi cha utendwa na irabu ishilizi. Licha ya kuwepo kwa muundo huo wa majina ya mahali kwa hakika majina ya aina hiyo siyo mengi. Kati ya majina ya mahali yaliyokusanywa katika maeneo yote yaliyoteuliwa lilipatikana jina moja tu lenye muundo huo. Tazama mfano ufuatao:

Ki-ta-twaar-w-a kisichotawaliwa
uk-K/kn-tdw-I

Kama tafsiri ya jina hilo ilivyo, watoa taarifa walifafanua kuwa kitongoji kinachoitwa Kitatwaarwa kilipewa jina na chifu (*Omukama*) kabla utaratibu wa kuvigawa vijiji katika sehemu ndogo zinazojulikana kama vitongoji. Ilelezwa kwamba jina hilo lilitokana na watu wa eneo hilo kuwa wakaidi kwani walikuwa siyo watii kwa chifu (*Omukama*). Kwa hakika muundo wa jina hilo unajidhihirisha kama kitenzi lakini umbo hilo linarejelea mahali, yaani kitongoji.

Katika makala haya tumefanya uchanganuzi wa vipashio mbalimbali vinavyounda majina ya mahali yenye muundo wa neno moja tu. Majina ya mahali yaliyochanganuliwa ni pamoja na majina ya mahali yenye muundo wa nomino na majina ya mahali yenye muundo wa kitenzi. Kwa ujumla, majina ya mahali ya Kihaya yenye muundo wa neno moja yanajidhihirisha katika ruwaza mbalimbali kama zilivyowasilishwa kwa muhtasari katika Jedwali lifuatalo:

**Jedwali 9: Muhtasari wa Ruwaza za Majina ya Mahali ya Kihaya**

| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | 9 | 10 | 11 | 12 | 13 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | ka- | | -baale | | | | | | | | |
| | | bu- | | -shasha | | | | | | | | |
| | | ki- | | -kanshe | | | | | | | | |
| | | mi- | | -gera | | | | | | | | |
| | | ka- | | -gab- | | -ir- | | | | -o | | |
| | | ka- | | -sher- | | -er- | | | | -o | | |
| o- | -mu- | -ki- | | -tuli | | | | | | | | |
| o- | -mu- | -ru- | | -baale | | | | | | | | |
| o- | -mu- | -i- | | -shuur- | | | | -an- | -ir- | -o | | |
| o- | -mu- | -i- | | -teer- | | | -ang- | -an- | -ir- | -o | | |
| o- | -mu- | -i- | | -mir- | | -ir- | -ang- | -an- | -ir- | -o | | |
| o- | -mu- | -ka- | | -shenye | | | | | | | | |
| a- | -ha- | -ki- | | -bati | | | | | | | | |
| | | bu- | | -gash- | | | | | | | -a | |
| | | bu- | | -tuura | | | | | | | | -ge |
| | | bu- | -ta- | -ganj- | | | | -an- | | | -a | |
| | | ki- | -ta- | -twaar- | -w- | | | | | | -a | |

**Ufunguo**

1. Kiambishi tangulizi
2. Kiambishi-ngeli cha mahali
3. Kiambishi-ngeli
4. Kiambishi cha ukanushi
5. Mzizi wa nomino/kitenzi
6. Kiambishi cha kutendwa
7. Kiambishi cha kutendea jambo cha kwanza
8. Kiambishi cha kutendana cha kwanza
9. Kiambishi cha kutendana cha pili
10. Kiambishi cha kutendea mahali
11. Kiambishi nomishi
12. Irabu ishilizi
13. Kiambishi elezi cha namna

## 5.0 Hitimisho

Makala haya yamewasilisha uchanganuzi wa vijenzi kuntu vinavyounda majina ya mahali ya Kihaya na kanuni zinazotawala vijenzi hivyo zimefafanuliwa. Kama ilivyoelezwa awali, uchanganuzi wa data katika makala haya umeongozwa na nadharia ya Mofolojia Leksika hususan mhimili wa ngazi Leksika. Uchanganuzi umebaini kuwa majina ya mahali ya Kihaya yanayojibainisha katika muundo wa neno moja moja yameundwa na vijenzi mbalimbali vilivyopangwa kidarajia msonge. Makala haya yamefafanua kuwa majina ya mahali yenye muundo wa nomino yamejibainisha katika miundo mitano tofauti ambayo ni: *muundo wa kiambishi-ngeli na mzizi, muundo wa kiambishi-ngeli, mzizi na kiambishi*

*nominishi*, *muundo wa kiambishi-ngeli, mzizi, kiambishi cha kutendea na kiambishi nominishi* na *muundo wa kiambishi tangulizi, kiambishi ngeli cha kwanza (mahali), kiambishi-ngeli cha pili na mzizi*. Muundo mwingine ni ule wa *kiambishi tangulizi, kiambishi ngeli cha kwanza (mahali), kiambishi-ngeli cha pili, mzizi, kiambishi cha kutendana, kiambishi cha kutendea na kiambishi nominishi*.

Ama kuhusu majina ya mahali ya Kihaya yenye muundo wa kitenzi, miundo mitano imejadiliwa. Majina ya mahali ya Kihaya yamejibainisha katika *muundo wa kiambishi cha upatanisho wa kisarufi, mzizi na irabu ishirizi*, *muundo wa kiambishi cha upatanisho wa kisarufi, kiambishi cha ukanushi, mzizi na irabu ishirizi* na *muundo wa kiambishi cha upatanisho wa kisarufi, mzizi, irabu ishirizi na kiambishi elezi cha namna*. Miundo mingine ni *muundo wa kiambishi cha upatanisho wa kisarufi, kiambishi cha ukanushi, mzizi, kiambishi cha utendwa na irabu ishirizi* na *muundo wa kiambishi cha upatanisho wa kisarufi, kiambishi cha ukanushi, kiambishi cha kutendana na irabu ishirizi*. Aidha, yafaa tuseme kwamba siyo kila kinachoitwa jina hujidhihirisha katika umbo la nomino kimofolojia. Baadhi ya majina ya mahali yenye muundo wa kitenzi yamethibitisha kuwa maumbo ya majina hayo siyo nomino bali ni vitenzi ingawa maumbo hayo yanarejelea mahali fulani.

## Marejeo

Agard, F. B. (1984). A *Course in Romance Linguistics: A Synchronic View*. USA: Georgetown University Press.

Angus, R. D. (2005). "Place Name Morphology and the People of Los Angeles." In *Caliphonia Linguistics Notes* Vol. 30.No. 2. p. 1 – 8.

Buberwa, A. (2010). Investigating Sociolinguistic Aspects of Place Names in Ruhaya in North-Western Tanzania. M. A. Dissertation (Unpublished), University of Dar es Salaam.

_______ (2011). "Viambishi-ngeli katika Nomino za Pekee: Mifano Kutoka katika Majina ya Mahali katika Kihaya". Katika *Jarida la Kiswahili*. Juz. 74. Kur. 41- 48.Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Byarushengo, E; Duranti, A. & Hyman, L. (1977) *Haya Grammatical Structure*. Los Angeles: University of Southern California.

Cameron, K. (1961) *English Place Names*. London: Batsford.

Dalby, D. (1984). Transcription of Ethnonyms and Toponyms in Afrika in Relation to their Historical Study. In *African Ethnonyms and Toponyms.* P. 11-17. Report and papers of the Meeting of Experts organized by UNESCO in

Paris 3-7 July, 1978. France: Imprimerie des Presses Universitaires de France, Vendome.

Diagne, P. (1984). Introduction to the Discussion of Ethnonyms and Toponyms. In *African Ethnonyms and Toponyms.* P. 11-17. Report and papers of the Meeting of Experts organized by UNESCO in Paris 3-7 July, 1978. France: Imprimerie des Presses Universitaires de France, Vendome.

Elihaki, Y. (2014). Majina ya Mahali katika Jamiilugha ya Chasu na Maana Zake.Tasnifu ya M.A (Haijachapishwa) Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Kadmon, N. (2000). Toponymy: *The Role, Laws and Languages of Geographical Names*. New York: Vantage Press.

Habwe, J. na Karanja, P. (2004). *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili*. Nairobi: Phoenix.

Kaji, S. (2000). *A Haya Vocabulary*. ILCAA: Tokyo University of Foreign Studies.

Kalkanova, T. (1999). "Sociology of Proper Names in Sofia Since 1970." In *International Journal of the Sociology of Language*. Vol. 135. p. 83 – 98.

Katamba, F. and Stonham, J. (2006). *Morphology*. Oxford: Blackwell. Lieber, R. (1990). *On the Organization of the Lexicon*. New York: Garland Publishing, Ink.

Leonard, G. (2008). Morphological Marking for Syntactic Relations in Ruhaya. Unpublished Dissertation. Dar es Salaam: University of Dar es Salaam.

Levitt, J. (1959). *The Spell of Words*. London: Darwen Finlayson.

Lieber, R. (1990). *On the Organization of the Lexicon*. New York: Garland Publishing, Ink.

Massamba D.P.B. (2004). *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*. Dar es Salaam: TUKI.

Mgullu, R. S. (1999). *Mtaala wa Isimu. Fonetiki, Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Mojapelo, M.L. (2009). "Morphology and Semantics of Proper Names in Northern Sotho". In *South African Journal of African Languages*. Vol. 2. p. 185-194.

Mphande, L. (2006). "Naming and Linguistic Africanism in African American Culture". In *Selected Proceedings of the 35th Annual Conference on African Linguistics*, ed. Mugane, J. p. 104-113. Somerville: MA: Cascadilla Proceedings Project.

Muzale, H.R.T. (2006). *Ikaningambo ya Oruhaya*. Dar es Salaam. Language of Tanzania Project. University of Dar es Salaam.

Nida, E. A. (1949). *Morphology: A Descriptive Analysis of Words.* Michigan: Michigan University Press.

Rugemalira, J.M. (2005). *A Grammar of Runyambo*. Dar es Salaam: Language of Tanzania Project, University of Dar es Salaam.

Rye, J. (2006). *A Popular Guide to Norfolk Place Names*. Guist Bottom: Larks Press.

Schotsman, P. (2003). *Place Names and History in Dar es Salaam*, Tanzania. Netherlands: Leaden University.